# Jaribio la Kuendesha gari: Cha kutarajia

WASHINGTON STATE DEPARTMENT OF LICENSING

Jaribio la kuendesha gari linapima uwezo wako wa kuendesha gari kihalali na salama. Mtahini anaabiri gari unaloendesha kutathmini uendeshaji wako wa gari. Hatajaribu kukuchanganya, kufanyia hila wala kukuomba kufanya chochote ambacho si halali.

## Nitajaribiwa nini?

Utajaribiwa kwa:

- **Kuanzisha gari lako.**
- **Kutoka maegeshoni,** je, unaweka ishara na ungoje hadi iwe salama kuingia katika msongamano wa magari?
- **Kudhibiti gari,** je:
  - Unatumia kanyagio la gesi, breki, usukani, na vidhibiti vingine sahihi?
  - Badili kasi yako kulingana na:
    - Nambari na kasi ya magari mengine na wanaotembea kwa miguu.
    - Hali ya barabara na anga.
    - Ujenzi.
    - Kiwango cha nuru.
    - Umbali unaoweza kuona mbele yako?
- **Kuendesha palipo msongamano wa magari,** je:
  - Unatumia njia sahihi?
  - Unaashiria ukitaka kubadili njia?
  - Unabadili njia kwa uangalifu?
  - Unafuata magari mengine kwa umbali salama?
  - Unageuza kichwa chako na kutizama nyuma kabla ya kubadili njia?
  - Unaashiria umbali sahihi kabla ya kugeuza?
- **Kutii ishara za trafiki,** je:
  - Unageukia njia sahihi bila kukata njia au kuenda pakubwa kwa njia isiyofaa?
- **Kuendesha gari kupitia makutano ambayo huwezi kuona kinachotendeka kwingine au palipo watu wengi,** je:
  - Unapeleleza kwa uangalifu kutambua ishara, wanaotembea kwa miguu au magari mengine?
  - Unasimamisha gari ili kuwawezesha madereva na wanaotembea kwa miguu kupita au kutumia haki yako ya njia sahihi?
- **Kusimama**
  - Unasimamisha gari vizuri na kwenye kituo sahihi?
  - Unaweza simamisha gari haraka na salama kukiwa na dharura?

# Jaribio la Kuendesha gari: Cha kutarajia

WASHINGTON STATE DEPARTMENT OF LICENSING

- **Kurudisha gari nyuma**
    - Je, unatizama nyuma kwa kutumia bega lako la kuume?
    - Unaweza kurudi nyuma kwenye mstari ulionyooka?
    - Una udhibiti mkamilifu wa gari lako?
- **Kukadiria umbali,** unabakia kwa umbali salama mbali na:
    - Magari mengine unapoyafuata au kuyapita, au
    - Watu wanaotembea au kuendesha baiskeli au pikipiki?
- **Kuheshimu haki ya wengine**
    - Je, una adabu kwa madereva wengine au wanaotembea kwa miguu au wenye baiskeli?
    - Je, unazingatia kikamilifu kazi yako ya uendeshaji gari?
- **Kufanya ujanja maalum,** unaweza kukamilisha yafuatayo kwa mafanikio?
    - **Ishara ya mkono ya kugeuka kushoto/kuume na kupunguza kasi na kusimama**. (Unaweza kutumia ishara ya mkono wakati wa majaribio.)
    - **Jaribio la mmenyuko wa breki/kusimama kwa dharura** – Tutakuelekeza kuweka mguu wako katika kanyagio la gesi na kukanyaga breki kwa haraka iwezekanavyo unapoambiwa usimame.
    - **Kuegesha mlimani** – Tutakuelekeza kuegesha gari lako kana kwamba utaliwacha bila kutunzwa.
    - **Kuegesh kwa sambamba** – Tutakuelekeza kurudi nyuma katika sehemu ya kuegesha, ama katikati ya:
        - Nguzo nne.
        - Magari mawili.
        - Au gari moja pamoja na gari la kudhani lililo umbali wa nusu urefu wa gari lililo nyuma.
        - Huwezi kutumia vipengele vya gari vya kusaidia kuegesha unapotekeleza ujanja wa kuegesha sambamba.
    - **Kuiga kurudi nyuma katika njia ya kuendesha gari au chochoro na kuingia kwenye msongamano wa magari kutumia kona** – Tutakuelekeza kurudisha gari lako nyuma karibu na kona kwa kuume. Unafaa kukaa karibu na ukingo wa barabara iwezekanavyo, na uendelee kwa usalama kurudisha gari nyuma kwa laini iliyonyooka hadi utakapoambiwa usimame. Unaweza kukosa kutumia kamera saidizi wakati wa ujanja wa kuiga kurudisha gari nyuma

# Jaribio la Kuendesha gari: Cha kutarajia

WASHINGTON STATE DEPARTMENT OF LICENSING

## Video hizi zinaweza kukusaidia

Unaweza kuzipata katika idhaa ya Department of Licensing YouTube
www.youtube.com/user/WALicensing

- Jaribio la Kuendesha Gari #1: Jaribio la awali
- Jaribio la Kuendesha Gari #2: Kuiga kurudisha gari nyuma
- Jaribio la Kuendesha Gari #3: Kuegesha kwa sambamba
- Jaribio la Kuendesha Gari #4: Kubadili njia na kugeuka

## Jiandae

Soma mwongozo wa Washington wa Madereva, na zaidi ya yote, fanya mazoezi. Kumbuka, unahitaji kufanya mazoezi na dereva mwenye leseni.

Unafaa kuwa na uepesi wa kuendesha gari kwa hali zote za trafiki. Jua sheria za barabarani na uzitii. Fanya majaribio kwa gari ulilozoea.

Kama watu wengine wengi, unaweza kuwa na woga kuhusu kufanya jaribio la kuendesha gari. Kama umefanya mazoezi na unakumbuka vidokezo vilivyoorodheshwa hapa na katika mwongozo wa madereva, una nafasi nzuri ya kupita jaribio la kwanza.

*Endesha gari salama na kila la heri!*